## Maradhi ya moyo yanazidi kuenea.

## Ndiyo kisababishi kikuu cha vifo miongoni mwa wanawake duniani kote.



Mradi huu unafadhiliwa na Chama cha Wagonjwa wa Zamani wa Taasisi ya Moyo ya Chuo Kikuu cha Ottawa..

# Dalili za mshtuko wa moyo hazitambuliki katika zaidi ya 50% ya wanawake.


**Dalili za kawaida zaidi za mshtuko wa moyo miongoni mwa wanawake:**

- Maumivu ya kifua, shinikizo, kubanwa au mchomo
- Maumivu kwenye taya, shingo, mkono wa kulia, au mgongo
- Kutokwa na jasho kupita kiasi
- Kupumua kwa shida
- Maumivu ya tumbo, kichefuchefu au tatizo la umeng'enyaji wa chakula

**Dalili zingine ambazo wanawake wanaweza kuhisi:**

- Udhaifu wa kupindukia
- Kukosa usingizi
- Kizunguzungu au kisunzi
- Mpigo wa moyo ulio wa kasi au usio wa kawaida

Mbali na maumivu ya kifua, wanawake wana uwezekano mkubwa wa kuwasilisha dalili 3 au zaidi.






Ukihisi kuwa anapatwa na mshtuko wa moyo, tafuta usaidizi mara moja. **Ikiwezekana piga simu 911. Usiendeshe gari.**

# Wanawake na wanaume wanaweza kuwa na aina tofauti za maradhi ya moyo.

**Aina ya maradhi ya moyo yanayopatikana zaidi:**

- Kuongezeka kwa kolesteroli katika mishipa ya moyo (maradhi ya ateri za moyo)
- Valvu za moyo zinazovuja au zilizo gumu (maradhi ya valvu za moyo)
- Mapigo ya moyo yaliyo kasi au yasiyo ya kawaida (arrhythmia)

**Wanawake wana uwezekano mkubwa wa kukumbwa na:**

- Kupasuka kwa ateri za moyo (spontaneous coronary artery dissection, SCAD)
- Ateri za moyo kuwa nyembamba na hivyo kuzuia damu kusonga (coronary vasospasm)
- Mishipa midogo kutofanya kazi (ugonjwa wa mishipa midogo)
- Moyo kudhoofika kwa sababu ya tukio linaloleta mafadhaiko (Takotsubo cardiomyopathy)
- Moyo kudhoofika wakati au baada ya ujauzito (peripartum cardiomyopathy)



Baadhi ya wahudumu wa afya huenda **hawajui tofauti hizi** baina ya wanawake na wanaume.



## Wanawake wanaweza kuwa katika hatari kubwa zaidi ya maradhi ya moyo.

**Hali zifuatazo husababisha hatari kubwa ya maradhi ya moyo:**

- Matatizo fulani ya ujauzito
- Kukoma hedhi mapema (kabla ya miaka 45)
- Ugonjwa wa uvimbe wa ovari na matatizo ya hormoni (polycystic ovarian syndrome)
- Magonjwa ya uvimbe na ya kinga nafsia (mfano. rheumatoid arthritis, lupus)
- Uvutaji sigara
- Ugonjwa wa kisukari

## Maradhi ya moyo yanaweza kuzuilika kwa kiasi kikubwa.

## Unafaa kufanya nini ili kuzuia hatari hiyo?

- Fanya mazoezi ili kudumisha afya bora.
- Kula vyakula mbalimbali vyenye afya.
- Dhibiti mfadhaiko.
- Ishi bila tumbaku ya dukani na uvutaji wa mvuke.
- Punguza pombe.
- Pima afya mara kwa mara (pimwa kiwango cha sukari kwenye damu, shinikizo la damu na kolesteroli).

ILI UWATUNZE WENGINE, NI LAZIMA KWANZA UJITUNZE WEWE MWENYEWE.

**ANZISHA MAZUNGUMZO HAYA.**

**Ili kuunga mkono, na kujifunza zaidi kuhusu afya ya moyo kwa wanawake, dalili, visababishi, hatari, na unachoweza kufanya, tembelea WearRedCanada.ca au zungumza na mtoa huduma wako wa afya.**

# MARADHI YA MOYO KWA WANAWAKE

## JE WAJUA?



WEAR**RED**CANADA.CA | @CWHH**ALLIANCE**

#MOYOWAKENIMUHIMU

CANADIAN WOMEN'S HEART HEALTH CENTRE | NATIONAL ALLIANCE

HER HEART MATTERS
WEAR RED CANADA • FEB 13